**JAMUHRI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MASASI**

**SHULE YA SEKONDARI CHIDYA**

S.L.P. 324

MASASI - MTWARA,

ChidyaSec@gmailcom,

Namba za simu

Mkuu wa Shule : 0784483628

Makamu Mkuu wa Shule: 0712921704

Mwalimu wa Taaluma: 0655398198

MZAZI/MLEZI WA ………………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI CHIDYA ILIYOPO WILAYA YA MASASI MKOA WA MTWARA KWA MWAKA 2022**

1.0. UTANGULIZI

Ninafurahi kukutaarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha tano shule ya sekondari Chidya, katika tahasusi ya …………….. hongera sana.
Shule ya sekondari chidya ipo umbali wa km.33 kaskazini kutoka makao makuu ya halmashauri ya Wilaya ya Masasi iliyopo mkoani Mtwara. Ili kufika Chidya sekondari Kuna basi ambalo hufanya safari kati ya masasi mjini na chidya kila siku, basi hilo huondoka
Masasi kati ya 6:30 -7:00 mchana kwa nauli ya Tsh 3,000/=Aidha watakao safari kwa gari binafsi au kama unatokea Dar es salaam unaweza kufika chidya sekondari kwa kuanzia
Chigugu au Namakongwa ambavyo ni vijiji vilivyopo kando ya barabara kuu itokayo Dar es salaam/Mtwara/Lindi kuelekea Masasi.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe ……………………………. Unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ………………. na mwisho kuripoti shuleni ni tarehe ………………….

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.0.ADA NA MICHANGO

a) Ada ya shule kwa mwaka ni Tsh 70,000/= ambayo ni sawa na Tsh 35,000/= kwa muhula. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya benki NMB.Jina la akaunti: Chidya secondaryschool Reccurent Account akaunti namba 70501200143"Tafadhali andika jina kamili la mwanafunzi kwenye pay - in- slip".

b) MICHANGO

i. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho iii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi na vibarua wengine. v. Shilingi 2000/= kwa ajili ya nembo ya shule
vi. Shilingi 15,000/= kwa ajili ya matibabu(Tsh 10,000/= kwa ajili ya bima ya afya na Tsh 5,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza) vii. Shilingi 20,000/= kwa ajili ya mitihani ya kujipima (Mock) viii. Mchango wa UMISETA Tshs. 3,000/=

Michango yote ilipwe benki katika benki ya NMB akaunti namba 70501200178 Jina la akaunti:Chidya secondary school self reliance account. "Tafadhali andika jina kamili la mwanafunzi kwenye pay - in- slip".

**2.1.SARE ZA SHULE**

i. Suruali mbili za rangi ya dark-blue unaweza kupata shuleni kwa Tsh.50,000/=@Tsh.25,000/= ii. Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu Tsh.30,000/=@Tsh.15,000/= iii. Jozi mbili za viatu vya ngozi rangi nyeusi
iv. Jozi mbili za soksi rangi nyeusi
v. Sweta moja rangi ya dark blue unaweza kupata shuleni kwa Tshs.15,000/=
vi. Tai dark - blue(ndefu saizi ya kati) unaweza kupata shuleni Tshs.3,000 vii. Mkanda mweusi wa ngozi unaweza kupata shuleni kwa Tshs 10,000/=

## 2.2. SARE ZA MICHEZO

1. Track - suit rangi ya kijani unaweza kupata shuleni kwa Tshs.25,000/=
2. Aje na Raba jozi moja za rangi yoyote.
3. Jezi za mpira wa miguu rangi ya nyeusi

## 2.3.SARE ZA KUSHINDIA

1. Suruali mbili za rangi nyeusi unaweza kupata shuleni kwa Tsh.50,000/=@Tsh.25,000/=
2. Tshirt mbili za rangi ya blue zenye kola zisizo na maandishi yoyote. Unaweza kupata shuleni kwa Tshs.30, 000/=@Tsh.15,000/=

NB. Nguo za aina nyingine yoyote tofauti na hizo hapo juu haziruhusiwi shuleni.

## 3.0.MAHITAJI MENGINE

i) Madaftari makubwa counter books ya kutosha , kalamu za wino, penseli, rula , mkebe, scientific calculator kwa wanafunzi wa masomo ya sayansi na dissecting kit kwa wanafunzi wanaosoma Baiolojia (Elimu ya viumbe) unaweza kupata shuleni vinauzwa

ii) Nauli ya mwanafunzi kwa ajili ya kuja shuleni na kurudi nyumbani wakati wa likizo.

iii) Aje na Godoro la sponji lenye upana wa ft $2^1/_2$ au unaweza kupata shuleni kwa Tshs.35,000/=

iv) Aje na Shuka mbili za rangi ya bluu.

v) Aje na Taulo moja

vi) Chandarua ya pembe nne kwa ajilli ya kujikinga na mbu unaweza kupata shuleni kwa Tshs.10,000/=

vii) Aje na Mto mmoja

viii) Aje na Kandambili jozi moja unaweza kupata shuleni kwa Tshs 2,000/=

ix) Aje na Vyombo vya chakula sahani, bakuli, kikombe , kijiko, dumu la lita tano kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa. Unaweza kununua shuleni.

x) Aje na Kivuli cha cheti cha kuzaliwa

xi) Ndoo mbili za ujazo wa lita 10 unaweza kupata shuleni kwa Tsh.5,000/=@2,500/=

xii) Aje na Sanduku imara(Tranka) la kuwekea vitu vyake

xiii) Aje na kivuli cha matokeo ya kidato cha nne (result slip)

xiv) Aje na Rimu mbili za karatasi za A4

xv) Wanafunzi wote waje na Vifaa vya usafi vifuatavyo unaweza kupata shuleni kwa gharama zifuatazo:-jembe tsh.7,000/=, mifagio ngumu na laini Tsh.7,000/=@3,500/=,sabuni ya maji lita 5 Tsh.7,500/=,fagio ya chelewa tsh.3,000 na mopa tsh.3,500/=kwa wanafunzi wa PCM na PCB waje na reki au unaweza kupata

shuleni kwa tshs.10,000/= na kwa wanafunzi wa CBG,HGL na HGK waje na panga au unaweza kupata shuleni kwa tshs.5,000/=
xvi) Fedha ya matumizi yake binafsi kwa muhula mzima.
xvii)Kwa wanafunzi wa PCB,PCM na CBG vifaa vifuatavyo vinaweza kununuliwa shuleni:-
(a)Scientific calculator Tsh.35,000/= (b)Disecting kit tsh.35,000/=
xviii)Aje na pasi ya mkaa kwa ajili ya kunyooshea nguo. xix)Awe na akaunti benki ya NMB kwa ajili ya kutumiwa pesa za matumizi.

## 3.1.**<u>SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII</u>**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na.25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha , inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo am bayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni - preparation
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndanin na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii. f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote
i) Kutunza mali za umma.
j) Kutii mabadiliko yoyote yatakayoathiri mabadiliko ya ratiba ya shule.
k) Marufuku kucheza lizangati eneo la shule

## 3.2.MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUMSABABISHIA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE. a)

Wizi

b) Usherati na ushoga

c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine , mirungi, kubeli na kadhalika. e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali za umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa.
h) Uvutaji wa sigara
i) Kufuga ndevu
j) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
k) Kukataa adhabu kwa makusudi
l) Kumiliki kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule
m) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa
n) Kutoa lugha chafu kwa walimu , wanafunzi wenzake, walezi na jamii kwa ujumla.
o) Kushiriki matendo ya uharifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.
p) Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
q) Kutembelea majumba ya starehe au nyumba za kulala wageni.
r) Kufanya jaribio lolote au kutishia kujiua kama kunywa sumu.

## 3.3.MAMBO MENGINE MUHIMU YANAPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI.

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni. b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na m akosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
d) Picha nne za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba zao za simu.

NB. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyateleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI CHIDYA**

**……………………………………**

**ZAWADI S. MDIMBE**

**MKUU WA SHULE**

**PRESIDENT'S OFFICE**

**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

Chidya secondary school
P.o.Box 324 MASASI
…………….... The

Medical Officer

……………………………………
…………………………………….
……………………………………

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**NAME OF STUDENT……………………………………………….**

Please examine the above named student to his fitness as indicated below. This certificate must be signed by a qualified Medical Officer of a Government hospital or Health centre.

1. Stool……………………………………………………
2. Urine……………………………………………………
3. Veneral Diseases………………………………………..
4. T.B…………………………………………………………
5. Eye……………………………………………………...
6. Ear…………………………………………………………
7. Chest…………………………………………………….
8. Abdomen……………………………………………….
9. Skin……………………………………………………...

10. Any other physical disability…………………………..

I certify that the above student is fit/not fit to pursue secondary education as indicated above.

NAME OF MEDICAL OFFICER…………………………………
SIGNATURE OF MEDICAL OFFICER………………………….
DESIGNATION…………………………………………………..
STATION……………………..OFFICIAL STAMP………………
DATE……………………………………….

**KUMBUKUMBU MUHIMU ZA MWANAFUNZI**

**(IJAZWE KABLA YA KURIPOTI SHULENI)** A.1.JINA

LA MWANAFUNZI…………………………………………..

Dini……………………………….Dhehebu…………………………….

2.(a)Jina la baba/mlezi …………………………….Passportsize (b)Kazi
ya baba,mlezi…………………………………………… **…….**
(c)Mahali anakoishi.
Kijiji/Mtaa…………………………..Kata………………..
Wilaya/Mji…………………………Mkoa………………..
Namba ya simu……………………Email…………………..WhatsApp…………………….

3.(a)Jina la mama/mlezi…………………………….Passportsize.
(b)Kazi ya mama,mlezi…………………………………………… **…….**
(c)Mahali anakoishi.
Kijiji/Mtaa…………………………..Kata………………..
Wilaya/Mji…………………………Mkoa………………..
Namba ya simu……………………Email…………………..WhatsApp……………………

**B.NDUGU WA KARIBU.**

| **Na** | **JINA** | **UHUSIANO** | **MAHALI ANAPOISHI** | **NAMBA YA SIMU** |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

NB:Njoo na picha za ndugu wote wa karibu

**<u>C.MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MGOMO/FUJO NA MAKOSA YA JINAI</u>**

Mimi…………………………………………..(mwanafunzi),naahidi kuwa
sitajihusisha/sitashiriki katika kupanga,kufanya wala kushabikia migomo,fujo au

ghasia zozote au  makosa ya jinai nikiwa Chidya sekondari katika muda wangu wa uanafunzi.
Sahihi…………………………………………..tarehe…………………………………….